# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA THELATHINI NA NNE

**28 MEI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**KIKAO CHA THELATHINI NA NNE - TAREHE 28 MEI, 2025**

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**432 MHESHIMIWA JONAS VAN ZEELAND (MVOMERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kujenga Shule ya Sekondari Kata ya Kikeo - Mvomero.

**433 MHESHIMIWA ERIC JAMES SHIGONGO (BUSHOSA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali inafahamu tatizo la uhaba wa Walimu hasa wa Masomo ya Sayansi nchini.

**434 MHESHIMIWA ASIA ABDUKARIMU HALAMGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Kata ya Endagau Jimbo la Hanang'.

**435 MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mkakati gani wa kuondoa upungufu wa Vituo vya Afya katika Kata za Tabora Mjini.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**436 MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Kiwanda cha Asali cha SAOHILL kilichopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kitanunua Asali kutoka kwa Wananchi.

## WIZARA YA FEDHA:

**437 MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Ofisi ya TRA katika Wilaya ya Mbulu.

## WIZARA YA UJENZI:

**438 MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali kupitia TANROADS itajenga kipande cha Barabara eneo la Matonga - Ifakara Mjini kama mchepuko wa Barabara kubwa ya sasa.

**439 MHESHIMIWA MWANTUMU DAU HAJI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itatengeneza Barabara ya Hombolo kwa kiwango cha lami ili iweze kupitika wakati wote.

**440 MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Njiapanda - Mang'ola - Matala hadi Lalago ambayo ipo kwenye Ilani ya CCM 2020/2025.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**441 MHESHIMIWA ATUPELE FREDY MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itapeleka Gari la Polisi Halmashauri ya Wilaya Busokelo.

**WIZARA YA KILIMO:**

**442 MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha zao la Pamba na Alizeti linastawishwa kisasa ili kuinua uchumi wa Wananchi Mkoani Simiyu.

**443 MHESHIMIWA NASHON WILLIAM BIDYANGUZE (KIGOMA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itajenga Skimu ya Umwagiliaji katika Mbuga ya Kalola Kijiji cha Nguruka - Uvinza.

**WIZARA YA MAJI:**

**444 MHESHIMIWA OLIVER DANIEL SEMUGURUKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, kuna mpango gani wa kuzipatia maji Kata za Ikuza, Mazinga, Kerebe, Goziba na Bumbire zilizopo Ziwa Victoria.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**445 MHESHIMIWA STEPHEN LUJWAHUKA BYABATO (BUKOBA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika jitihada zake za kuwekeza mtaji katika Kiwanda cha Kahawa cha TANICA - Bukoba Mjini.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**28 MEI, 2025** **KATIBU WA BUNGE**